



# TANGAZO ↔ TANGAZO

## TANGAZO LA KUKODI MAGARI KATIKA KAZI MAALUMU

TANGAZO NAMBA: LGA/177/2023/2024/HQ/NC/35/01

Tarehe 16/08/2023


### MAELEZO YA TANGAZO

1. Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imepatiwa fedha na Serikali kuu kwa ajili ya shughuli za Mitihani ya kumaliza Elimu ya msingi kwa mwaka 2023 na inakusudia kutumia baadhi ya fedha zake kukodi magari.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Itigi inakaribisha maombi kwa wenye magari yenye uwezo wa kufanya kazi ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kuanzia tarehe 12.09.2023 hadi 14.09.2023.
3. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha kwenye barua yake ya maombi nakala za nyaraka zifuatazo;
  - 3.1 Namba za usajiri wa gari
  - 3.2 Aina ya mafuta yatakayotumika kwenye gari hilo
  - 3.3 Uwezo wa gari wa kubeba watu wasiopungua wanane (8) pamoja na mizigo muhimu
  - 3.4 Uhai wa Bima ya gari na ulipiaji wa mapato ya TRA

- 3.5 Uhai wa Leseni ya dereva anayeendesha gari hilo
- 3.6 Namba za simu za mwenye gari kwa ajili ya mawasiliano
4. Halmashauri itatoa mafuta (Dieseli au Petrol) ya gari kulingana na umbali wa safari isipokuwa vifaa vya kiufundi kwa ajili ya gari litakuwa la mwenye gari
5. Mwombaji awe tayari kufanya kazi popote katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Itigi
6. Gharama ya kukodi gari itakuwa ni TZS 100,000.00 kwa siku kwa kila gari kwa siku tatu (3) yaani TZS 300,000.00 kwa siku tatu (3).
7. Barua ya maombi iandikwe vizuri na kusainiwa na mwombaji.
8. Kamati ya wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi itafanya zoezi la tathimini ya nyaraka zitakazowasilishwa.
9. Barua zote za maombi zitumwe kwa;

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,  
S.L.P 70,  
ITIGI.**

10. Barua zitakazotumwa kwa njia ya posta au barua pepe hazitapokelewa
11. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 25.08.2023 saa 04:00 Asubuhi na barua zitafunguliwa siku hiyo hiyo katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

  
MKURUGENZI MTENDAJI  
John K. Mgalula HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**